# TAARIFA KWA UMMA

Imebainika kuwepo kwa watu au makundi ya watu yanayoshawishi wananchi kutotoa ushirikiano kwa Tume ya Uchunguzi, ikiwemo kutoa maoni, ushahidi au taarifa kwa namna yoyote ile. Ushawishi huo hausaidii jitihada za kitaifa za kutafuta ukweli, haki, kujifunza kutokana na yaliyopita na kuweka msingi wa suluhu ya kudumu.

Wananchi wanashauriwa kupuuza ushawishi wowote unaolenga kuwazuia kushiriki, na badala yake watoe maoni na ushauri kwa Tume. Kupitia sauti za wananchi, Taifa linaweza kutambua changamoto zilizojitokeza, kuzitatua na kuchukua hatua za kuhakikisha matukio kama hayo hayajirudii siku zijazo.

Tume ya Uchunguzi ipo kwa ajili ya Watanzania wote, na mafanikio ya kazi yake yanategemea ushiriki mpana, wa hiari na wenye uwazi kwa wananchi. Amani, mshikamano na mustakabali salama wa Taifa letu ni jukumu la kila mmoja wetu.

Tume ya Uchunguzi

Scan kutoa maoni yako hapa

26 Desemba, 2025

**Imetolewa na**
**TUME YA UCHUNGUZI**

www.tume.uchunguzi.go.tz 0743 040 890